Halmashauri ya Mji Geita
GEITA
TOWN COUNCIL

# GEITA LEO
## TOLEO LA 12

JARIDA LA | OKTOBA - DISEMBA ,2022









# SALAMU ZA MWAKA 2023 KUTOKA KWA VIONGOZI

Ndugu wananchi wa Wilaya ya Geita, awali ya yote tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kumaliza mwaka 2022 salama tukiwa na afya njema ya mwili na roho, na kutuvusha mpaka mwaka mpya wa 2023. Tutumie fursa ya jukwaa hili kuwashukuru kwa dhati kwa namna mlivyoshirikiana na Halmashauri ya Mji wa Geita katika kuhakikisha tunafanikisha shughuli mbalimbali za utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kuendelea kulipa na kutoa kodi ambazo zimetuwezesha kukusanya mapato ya Halmashauri kwa asilimia 105.85% mwaka wa fedha 2022/2023 na kuvuka malengo tuliyokuwa tumejiwekea.

Tunatoa shukrani za dhati kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutuwezesha kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika sekta za Afya, Elimu, Kilimo na Mifugo, Utawala bora nk. Kubwa Zaidi tunaishukuru Serikali yetu tukufu kwa kutuwezesha Shilingi Bilioni 1.4 zilizotuwezesha kujenga vyumba vipya 71 vya Madarasa kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza 2023 katika Shule za Sekondari Mkangala,Bulela, Ihanamilo, Kisesa, Nyanguku, Nyabubele, Mwatulole, Kalangalala, Bombambili, Lukaranga( Mkolani), Kivukoni na Shantamine. Serikali yetu imetufanyia jambo la Fahari ambalo litaendelea kukumbukwa kizazi mpaka kizazi, tunawasihi wazazi na walezi wote ambao mna Watoto waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza 2023 mhakikishe mnawapeleka shule wanafunzi hao ili wakaanze masomo, pia Watoto wote waliofikisha umri wa kuandikishwa elimu ya awali na Darasa la kwanza wapelekwe shule pasipo kuwaficha Watoto wenye ulemavu wa aina mbalimbali kwani kupata elimu ni moja ya haki ya msingi ya mtoto.

Tunapenda kuwatakia heri na baraka ya Mwaka mpya 2023 na kuwasihi kuendelea kujitoa kwa hali na mali katika kuhakikisha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika Halmashauri ya Mji wa Geita unafanikiwa kama ilivyokusudiwa ikiwemo nguvu kazi katika ujenzi wa miradi, kujitokeza kushiriki katika kampeni mbalimbali kama upandaji miti, usafi wa mazingira na mengineyo, kuendelea kuunga mkono Timu yetu ya mpira wa miguu ya Geita Gold FC ambayo inashiriki ligi kuu ya Tanzania bara na kuendelea kudumisha ulinzi na usalama katika jamii yetu.

Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Ibariki Geita.
Kazi Iendelee

## POCHI LA MAMA

Mnamo mwezi Oktoba 2022 Serikali yetu tukufu inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliipatia Halmashauri ya Mji Geita kiasi cha Tsh.1,420000 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 71 vya madarasa ya kidato cha kwanza 2023, ambapo kila darasa limegharimu shilingi Milioni 20 zikiwemo Meza na Viti 50 kwa kila darasa. katika shule 12 zilizopo kwenye kata mbalimbali za halmashauri ya Mji Geita.



## VYUMBA 10 VYA MADARASA KISESA SEKONDARI



## VYUMBA 9 VYA MADARASA KALANGALALA SEKONDARI



## VYUMBA 9 VYA MADARASA BOMBAMBILI SEKONDARI



## VYUMBA 9 VYA MADARASA LUKARANGA SEKONDARI



## VYUMBA 7 VYA MADARASA MKANGALA SEKONDARI



# VYUMBA 7 VYA MADARASA MWATULOLE SEKONDARI



# VYUMBA 7 VYA MADARASA SHANTAMINE SEKONDARI



## VYUMBA 5 VYA MADARASA KIVUKONI SEKONDARI



## VYUMBA 3 VYA MADARASA BULELA SEKONDARI



# VYUMBA 2 VYA MADARASA IHANAMILO SEKONDARI



# VYUMBA 2 VYA MADARASA NYABUBELE SEKONDARI



## CHUMBA 1 CHA DARASA NYANGUKU SEKONDARI



## MEZA NA VITI 50 KILA DARASA



## HABARI KATIKA PICHA



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Geita Bi. Zahara Michuzi akikagua maendeleo ya Ujenzi wa Madarasa ya wanafunzi wa kidato cha kwanza 2023

## HABARI KATIKA PICHA

wasichana waliorejea shuleni kuendelea na Elimu ya watu wazima (SEQUIP) baada ya kukatisha masomo katika mfumo rasmi kutokana na sababu mbalimbali wakitoa burudani ya Ushairi wakati wa Maadhimisho ya Juma la Elimu ya watu wazima yaliyofanyika kiwilaya katika viwanja vya CCM Kalangalala Mwezi Novemba 2022



## MRADI WA MAJI MANGA

Mradi wa Maji Manga Kata ya Mgusu ambao unatekelezwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Kupitia kwa fundi mzawa .
Mradi huu utakapo kamilika utahudumia watu 3241 wa Mtaa wa Manga na maeneo ya jirani na unakadiriwa kutumia kiasi cha Tsh. 252,419,085.481.



## MRADI WA MAJI MANGA

Mmoja wa wa wananchi wa Mtaa wa Manga akipata huduma ya maji safi na salama katika kisima kilichopo katika Mtaa wake.



## KIVUTIO CHA KIHISTORIA

Moja ya Choo kilichokuwa kinatumiwa na Wahunzi enzi za utawala wa wakoloni (wajerumani) jengo hili mpaka sasa linapatikana katika Mtaa wa Lwenge Kata ya Kalangalala Geita Mjini



## HABARI KATIKA PICHA




Mbunge wa Jimbo la Geita Mjini Mhe. Costantine Kanyasu akizungumza na wananchi pamoja na Wanafunzi (hawaonekani pichani) wakati wa maadhimisho ya siku ya Ukimwi Duniani yaliyofanyika katika Shule ya Sekondari Shantamine.

## HABARI KATIKA PICHA

Mkuu wa Mkoa wa Geita Mhe. Martine Shigela (aliyevaa kofia ) akikagua Shughuli zinazofanywa na chama cha wanawake wachimbaji wa Madini Mkoa wa Geita alipotembelea banda lao wakati wa Maonesho ya tano ya Kitaifa ya Madini yaliyohitimishwa mwezi Oktoba 2022 katika viwanja vya EPZ Bombambili Mjini Geita



## HABARI KATIKA PICHA

Mkurugenzi mtendaji wa Mgodi wa Dhahabu wa Geita Bw. Terry Strong (aliyesimama kulia) akiwa kaika picha ya pamoja na Makamu Mwenyekiti wa Timu ya Mpira wa Miguu ya Geita Gold Football Club (GGFC) Ndg. Zengo Polle (aliyesimama kushoto) baada ya kusaini Mkataba wa makubaliano ya kuwa wadhamini wakuu wa timu hiyo kwa mwaka 2022/2023.



## MADARASA KIVUKONI

Mradi wa Ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa, Ofisi ya walimu na matundu sita ya Vyoo vya wanafunzi ambao umetekelezwa kwa Tsh. 73,576,684.02 ambazo zimetolewa na mfuko wa jamii nchini **(TASAF)** pamoja na nguvu za wananchi



## KIVUTIO CHA KIHISTORIA

Chemchemi ya Maji Lwenge ambayo Maji yake nisafi na hayakauki kipindi chote tangu enzi za Mkoloni. inatoa huduma ya Maji kwa wakazi wengi katika mji wa Geita pia inasemekana kuwa eneo hilo lina nyoka mkubwa ambaye huwa anatokea mara chache kutoka chanzo cha maji kilipo alimaarufu Keita Abantu (Mlimani)





## BWENI LA WANAFUNZI



Ujenzi wa Bweni la Wanafunzi katika Shule ya Sekondari Geita, Bweni hilo lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 80 limejengwa kwa Tsh.Milioni 100 kutoka Serikali kuu kupitia Programu ya Lipa kulingana na matokeo (EP4R).

## UJENZI WA BARABARA

Ujenzi wa kalavati mbili barabara ya Lukaranga Sekondari hadi Shinde ukiwa umekamilika. Shughuli hii imetekelezwa na wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) Wilaya ya Geita.



## NYUMBA YA WALIMU

Nyumba pacha ya walimu (Two in One) katika shule ya Msingi Manga Kata ya Mgusu ambayo imejengwa kwa nguvu za Wananchi na Halmashauri iliwapatia Tsh milioni 30 kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya ukamilishaji.



## VYOO BORA

Choo cha wanafunzi chenye matundu 20 katika Shule ya Msingi Samina ambacho kimejengwa kwa Tsh. milioni 33 kupitia nguvu ya Wananchi wa Mtaa wa Samina.



## ZAHANATI YA BWIHEGULE

Mradi wa ujenzi wa Zahanati ya Bwihegule kata ya Mtakuja ambao ulipatiwa Tsh. Milioni 100 kwaajili ya ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje na nyumba moja ya Mtumishi kupita Fedha za CSR kutoka mgodi wa GGM..



## MAISHA GROUP - GEITA

Vijana wanaounda kikundi cha Maisha Group kinachopatikana kata ya Nyankumbu ambao wanajishughulisha na utengenezaji wa mikanda ya Gypsum wanakikundi hawa wamenufaika na mkopo isyo na riba inayotolewa na Serikali kwa makundi maalum



## MRADI WA KILIMO

Mradi wa uanzishaji kitalu miche ya Korosho na Parachichi ambapo kwa jumla umegharimu Tsh. milioni 15,350,000 za mapato ya ndani ya Halmashauri. matarajio ya Mradi huu ni kuwahamasisha wakulima kupanda Mazao hayo katika Wilaya ya Geita kwa sababu nimazao ya kibiashara ya kudumu



## ZAHANATI NAKAHENGELE

Wajumbe wa kamati ya Siasa Wilaya ya Geita wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Geita Barnabas Mapande wakikagua ujenzi wa Zahanati ya Nyakahengele Kata ya Ihanamilo ambayo inajengwa kupitia fedha za huduma ya kampuni kwa Jamii (CSR) kutoka Mgodi wa GGM.



# KITUO CHA AFYA BULELA



# KITUO CHA AFYA BULELA

Ujenzi wa Majengo matatu ambayo ni Maabara, Wodi ya wazazi na Jengo la upasuaji katika Kituo cha Afya Bulela. Majengo haya yamejengwa kwa Tsh Milioni 400 za Mapato ya ndani ya Halmashauri ya Mji wa Geita.







# HALMASHAURI YA MJI GEITA

**Jarida hili hutolewa bure kila baada ya miezi Mitatu na Kitengo cha Mwasiliano Serikalini, Halmashauri ya Mji wa Geita.**

S.L.P 384 Geita Simu Na. **0282520437.**
Nukushi Na. **0282520347**
Barua pepe : **td@geitatc.go.tz** Tovuti : **www.geitatc.go.tz**